



# Davis School District

LEARNING FIRST

## BARUA KWA WAZAZI KUHUSU RIDHAA YA MAHOJIANO/ UPIGAJI PICHA NA KUREKODI VIDEO

Kwako Mzazi,

Miongoni mwa jitihada za shule ya Davis School District kimawasiliano ni kuuhabarisha umma juu ya shughuli za kielimu zinazoendelea katika mandhari ya shule yetu.

Ni katika jitihad hizi, walau mara chache huwaalika wanahabari shuleni kuchukua habari za shughuli na matukio mbalimbali ya kielimu shuleni kwetu.

Walengwa wakuu wa elimu, bilashaka huwa ni wanafunzi na muda mwingi sisi na wanahabari hupenda kuwalenga wanafunzi kama chanzo cha habari hizo.

Kwa maana hiyo, tunaomba ridhaa yako mapema ili mtoto wako aweze kuhojiwa, kupigwa picha na kuchuliwa video katika matukio na shughuli za kielimu pale fursa itakapojitokeza katika mwaka huu wa masomo. Hii itajumuisha katika matumizi ya tovuti ya shule pamoja na akaunti za mitandao ya kijamii. Tafadhali zingatia, sera za Davis School District zinazuia matumizi ya jina kamili la mwanafunzi katika picha au video katika matumizi yoyote ya kishule.

Kuna wakati mamia ya wanafunzi wanakuwa pamoja viwanjani, bwaloni au katika namna yoyote ya mkusanyiko. Katika hali hii tutafanya kila liwezekanalo kutambua ni mwanafunzi gani anavuka mipaka kitabia wakati wa mikusanyiko kama hiyo. Hata hivyo, mikusanyiko kama hii huwenda ikawa changamoto katika kudhibiti hilo.

Pia, kama mwanafunzi anashiriki katika matamasha makubwa nje ya shule kama vile kwaya, michezo au tamasha lolote, hairuhusiwi kuondolewa (katika picha au video).

Kama **HUTAKI** mtoto wako kushirikishwa katika moja ya/ au vipengele vyote, tafadhali jaza fomu hii na uirejeshe shuleni. Tambua kuwa, itahesabika kuwa umetoa ridhaa endapo hutowasilisha fomu hii shuleni.

Tafadhali bainisha ni vipengele gani usingependa kuvijumuisha: Andika **NARUHUSU** au **SIRUHUSU**

\_\_\_\_\_ Mtoto wangu KUPIGWA PICHA na kurekodiwa kwa matumizi ya shule.

\_\_\_\_\_ Mtoto wangu KUPIGWA PICHA, na kurekodiwa na kuhojiwa na mtu wa nje wala Mwanahabari.

Jina la mtoto: \_\_\_\_\_

Jina la mzazi: \_\_\_\_\_

Anwani: \_\_\_\_\_

Namba ya simu: \_\_\_\_\_

Saini: \_\_\_\_\_

Tarehe: \_\_\_\_\_